| | | |
|---|---|---|
| EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE | **OMBI LA KUTOA HUDUMA:<br>UTOAJI HUDUMA MBALIMBALI KWA MKANDARASI MKUU WA USIMAMIZI WA UENDESHAJI MRADI WA BOMBA LA MAFUTA (EACOP)<br>KUMBUKUMBU REJEA NAMBA. EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01** | EALS LTD |

E.A.L.S Limited Tanzania ni Mkandarasi Mkuu wa Usimamizi wa Utekelezaji wa Mradi wa EACOP, anayakaribisha mashirika yenye uzoefu na sifa bainifu yaliyo tayari kutoa huduma mbalimbali kulingana na maelezo ya mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba linalopita ardhini na linalovuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale wilayani Hoima, Uganda, hadi Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati ya hizo kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

## MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA ZINAZOHITAJIKA

| Namba ya kumbukumbu | Maelezo |
|---|---|
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0001 | Vifaa vya TEHAMA (Kompyuta za mezani, kompyuta mpakato, vifaa vya mkutano) |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0002 | Huduma na vifaa vya ushikiliaji na ubebaji |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0003 | Ununuzi wa Magari (gari la abiria la ukubwa wa 4x4 na pick-up) |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0004 | Uhifadhi wa bomba na Mfumo wa Usafiri |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0005 | Huduma za Simu za Mkononi |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0006 | Ofisi za kuhamishika, sehemu za kuhifadhi bidhaa katika baridi (futi 40) na makambi. |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0007 | Jenereta za umeme zinazohamishika (15 - 40 Kva) |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0008 | Huduma za Kuzima moto na Usalama |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0009 | Shughuli za ujenzi (Morogoro,Dodoma, Singida, Muleba, Mutukula, Tanga, Katesh, Babati, Mwanga, Isaka) |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0010 | Ugavi wa Vipimo vya kuongeza kasi (Kinasa Mshtuko) |
| EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI 0011 | Ugavi wa usalama mahala pa kazi (PPE) |
| EALS-TZA-OG-PRC-F- 0001 REV 01 EOI 0012 | Mifumo ya kielektroniki ya ufuatiliaji mizigo, Mfumo wa WMS kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa kwa wateja. |

**MAHITAJI YA KIWANGO CHA CHINI:** Kampuni zenye nia ya dhati zinaalikwa kuwasilisha nyaraka zao zikiambatana:-

- Uthibitisho wa usajili kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania na Cheti cha Kuidhinisha Kodi cha (TRA) kwa mwaka wa hivi karibuni.
- Usajili uliokamilika wa Mtoa Huduma kwa Wagavi wa EWURA (LSSP) unapendekezwa sana.
- Kuzingatia Kanuni za Maudhui ya Ndani, 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya Ndani.
- Marejesho ya mwaka ya karibuni pamoja na risiti ya malipo
- Nakala za vitambulisho vilivyotolewa na serikali kwa wanahisa wote
- Uthibitisho wa ISO na tasnia husika; sera na taratibu za kampuni yaani HSE, AML, Haki za Binadamu n.k.
- Cheti cha uanzishwaji/usajili wa kampuni kutoka kwa msajili wa makampuni (BRELA)
- Hati ya makubaliano na Kanuni ya kampuni;
- Cheti cha TIN; Leseni na Vibali halali vyote vya Biashara;
- Taarifa za ukaguzi wa fedha za karibuni;
- Marejeleo ya sasa na ya zamani; uzoefu husika, Uthibitisho wa bima Na Miradi ya zamani ya uwajibikaji kwa jamii.

**Ili kupokea maelezo ya kina ya maombi ya utoaji huduma zilizotajwa hapo juu**, Kampuni ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa katika sehemu iliyo hapo juu kupitia barua pepe kwa **suppliers@eals. co.tz** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) kabla au saa 09:00 mchana kwa Saa za Afrika Mashariki (EAT) Februari 23, 2022 na tarehe ya mwisho ni siku kumi na nne baada ya chapisho la kwanza. Kichwa cha barua pepe kinapaswa kusomeka kama ifuatavyo: **EALS-TZA-OG-PRC-F-0001 REV 01 EOI (Nambari ya marejeleo) & EOI (Jina).**

**Kumbuka:** E.A.L.S Limited itakagua na kutathmini nyaraka zinazotolewa na kampuni zilizoonyesha nia ili kupata orodha ya kampuni zilizopita katika mchujo wa kwanza. Kampuni zilizokidhi vigezo pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni ili kuendeleza na mchakato wa zabuni, kwa kuzingatia kanuni ya Utunzaji wa Taarifa Nyeti (NDA). Nyaraka zote za maombi ya zabuni zinatakiwa kuwasilishwa kwa lugha ya Kiingereza.

**E.A.L.S Limited inayo haki ya kutozichagua kampuni ambazo zinawasilisha ripoti zisizokamilika.**